
# Kijitabu cha Maelezo kwa Wafugaji wa Ngamia



## Ufugaji bora wa Ngamia

VÉTÉRINAIRES
SANS FRONTIÈRES
SUISSE
member of VSF International

biovision

# Kijitabu cha Maelezo kwa Wafugaji wa Ngamia

## Ufugaji bora wa Ngamia

VSF
VÉTÉRINAIRES SANS FRONTIÈRES SUISSE
member of VSF International

ISIOLO COUNTY GOVERNMENT
Peace and Prosperity

biovision

Veterinaires Sans Frontieres Suisse na Idara ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi Kaunti ya Isiolo

Kitabu cha mwongozo wa ngamia kwa wafugaji, wachungaji na waekezaji.

Toleo la kwanza

ISBN No. 978-9914-49-227-9
Machi 2022.

## MAENDELEZO

Ngamia wanahistahimili mazingira magumu ya maeneo kame au nusu kame. Wanyama hawa wamefugwa kwa karne nyingi na jamii mbalimbali za wafugaji katika eneo kubwa pembeni mwa Afrika. Jinsi  athari za mabadilko ya hali ya anga yanavyo onekana kwa dhahiri, ndivyo ukulima  bunifu unao kubali mabadiliko hayo hauwezi epukika duniani kwote.

Nchini Kenya, ufugaji wa ngamia umekuwa ukiongezeka kwa kila uchao kwa zile jamii ambazo hazikuwa zinawafuga kama moja wapo ya njia za kukabiliana na mabadiliko ya hali anga. Idadi ya ngamia katika kaunti ya Isiolo ni 148,000. Maziwa ya ngamia ni lishe bora, ni njia ya mapato na pia hupatikana hata wakati wa kiangazi ambapo maziwa kutoka kwa mifugo wengine hayapatikani, hasa maeneo kame. Kama vile msemo wa kale unavyosema "Maarifa ni nguvu", vitabu vya mafundisho tofauti tofauti kuhusu ufugaji wa ngamia, afya ya ngamia na usafi wa maziwa vimechapishwa, ila hakuna vile vimeandikwa katika lugha ambayo inaeleweka  vizuri kwa wafugaji, wachungaji na wafanyabiashara ya maziwa  ambao hawana masoma au wana masomo ya kiwango cha chini.

Mwongozo huu umeundwa na VSF-Suisse wakishirikiana na Kaunti ya Isiolo Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, ili kujaribu kuziba pengo hili. Mwongozo huu unanuiwa kutumiwa na wadau wote ili kuboresha ufugaji  wa ngamia, afya yake, usafi  wa maziwa, kupunguza hasara ya maziwa, kuboresha usalama wa maziwa ya ngamia kwa matumizi ya binadamu, na pia kuzidisha mapato kwa thamani ya maziwa. Kitabu hiki cha mwongozo wa picha kimeandikwa kwa lugha ya kiswahili na ni thibitisho muhimu kwa wafanyakazi wa ugani na wadau wote waliopo katika uborashaji wa  thamani wa ngamia.

Mwongozo huu umeundwa  kama sehemu ya mradi wa ngamia uliotekelezwa na VSF-Suisse wakishirikiana na Serikali ya Kaunti ya Isiolo kutoka mwaka wa 2010-2022. Utachangia uborashaji wa ufugaji wa ngamia katika kaunti ya Isiolo na kwingineko.

Dkt. Lawrence Mwongela,
Waziri wa kilimo, Ufugaji na Uvuvi, Kaunti ya Isiolo

## KUKIRI

Ningependa kuutambua msaada wa kifedha uliotolewa na Biovision Foundation for Ecological Development, waliofadhili mradi kwa jina; (Upscaling of Integrated Camel Management for livelihoods and collaborative disease surveillance for Animal Health in the climate-change Affected ASAL Region of Kenya)-UPICAM II, Mradi nambari BV DPA-002. Lau sivyo haingewezekana kuchapishwa kwa kijitabu hiki cha mwongozo. Kufanikiwa kwa kitabu hiki cha mwongozo ni kwa juhudi za watu mbalimbali walioshiriki.

Shukrani za dhati ziwaendee watu wafuatao waliojitolea kuhakikisha ufanisi wa mwongozo huu: Kutoka Serikali ya Kaunti ya Isiolo ni Bw. Wallace Kingori kutoka Idara ya huduma ya afya ya mifugo; Bw. Dickson Chaulo na Bw. Bernard Wafula kutoka Idara ya maendeleo ya mifugo; Bw. Muktar Ibrahim, Bw. Francis Lekapana na Bi. Genevieve Owour kutoka VSF-Suisse; Waalimu wa kiswahili Bi. Edith Kajuju Mwogera na Bw. Ali Akunda wa wizara ya elimu, Isiolo,Kenya.

Tunatambua kutumika kwa sehemu ya uandishi wa Marejeo katika kitabu hiki.

Dkt. Davis Ikiror,
Mkurugenzi wa Nchi (Kenya-Somalia), VSF-Suisse

## KANUSHO

Nakala hii imetolewa kwa usaidizi wa kifedha kutoka kwa Biovision Foundation for Ecological Development. Yaliyomo kwenye hati hii ni kwa mujibu wa waandishi na hivyo basi Biovision na VSF Suisse wanajitenga na msimamo wowote ambao umeonekana au kudhihirika katika hati hii.

Hakimiliki©
Vétérinaires Sans Frontières Suisse (VSF-Suisse),
Barabara ya Muthangari, Kando ya Barabara ya Gitanga, MCK Jumba la Synod Nairobi, Lavington.
S.L.P 25656 - 00603,Nairobi.
Baruapepe: Office.Nairobi@vsf-suisse.org, Tovuti, www.vsf-suisse.org,
Nambari ya simu ya rununu, +254 721 551 024

## HAKI ZIMEHIFADHIWA NA KUSHIRIKISHWA

Toleo hili huenda likachapishwa, likatolewa nakala, likahifadhiwa kwa mfumo wa kurejesha au kusambazwa kwa namna yoyote ile au kwa njia za kielektroniki, kimitambo, likanakiliwa, likarekodiwa au namna nyingine, lakini likiwa limebakia jinsi ilivyo na nembo na majina ya waandishi, wachapishaji, waliobuni na pia mashirika husika.


Toleo hili si la kuuzwa wala kutumiwa kwa nia za kibiashara ili kupata faida. Idhini ya uchapishaji na usambazaji wa nakala hizi ni kupitia kwa VSF-Suisse Nairobi. Idhini ya uchapishaji lazima ipeanwe kwa njia ya maandishi kutoka kwa waandishi na mchapishaji, mwombaji ndiye atakayesimamia gharama zote za kuchapisha na kusambaza ikiwemo nembo za shirika husika pamoja na ufadhili wa uchapishaji.

Kimeundwa na kuchapisha na kampuni ya Zoli Creation, Mchoraji wa Picha ni Simon Ndonye,
S.L.P: 51217 00200, Nairobi Kenya, simu:+254 722 245 957, Baruapepe: ndonyesimon@gmail.com,
Tovuti: www.zolicreation.com
Kimehaririwa na: Dkt.Davis Ikiror

# Jedwali la Yaliyomo

1. MAENDELEZO....................iii
2. UFUGAJI BORA WA NGAMIA....................1
3. UZALISHAJI WA NGAMIA....................3
4. NGAMIA ANAPOZAA....................5
5. JINSI YA KUTUNZA NDAMA....................7
6. JINSI YA KUMPATIA NGAMIA LISHE BORA....................9
7. AFYA YA NGAMIA....................11
8. JINSI YA KUPATA MAZIWA SAFI YA NGAMIA....................13
9. MAREJELEO....................15


# UFUGAJI BORA WA NGAMIA



MAELEZO KWA MFUGAJI ILI AWEZE KUPATA MAZAO ZAIDI


## UTANGULIZI

Ngamia ni mfugo anayepatikana katika maeneo kame au nusu kame. Ngamia ana uwezo wa kula majani ya miti tofauti hadi urefu wa mita mbili unusu na pia hula nyasi.



Ngamia ana uwezo wa kutoa maziwa kwa kipindi cha mwaka mzima hata akiwa amebeba mimba; pia huendelea kutoa maziwa hata wakati wa kiangazi ambapo mifugo wengine kama ng'ombe huacha. Ngamia anauwezo wa kumpa mfugaji maziwa lita sita kwa wastani kila siku. Ngamia mmoja wa kike hutoa maziwa mara tano hadi kumi ukilinganisha na ng'ombe katika kipindi kimoja cha utoaji wa maziwa wakiwa wote katika mazingira ya ukame na joto.


Kwa kuwa ngamia ula miti mbalimbali, inaaminika kuwa maziwa yake hutumika kuyatibu magojwa mbalimbali kama vile kisukari na shinikizo la damu. Maziwa haya pia yanakiwango cha juu cha vitamini 'c' ambayo ni muhimu kwa afya ya binadamu. Maziwa ya ngamia yana soko nzuri.



Maziwa ya ngamia yana soko nzuri kuliko maziwa ya mifugo wengine; lita moja ya maziwa haya huwa na bei ya juu ikilinganishwa na ya mifugo wengine.

Mapato kutoka kwa uuzaji wa maziwa haya ni mengi, kwa mfano: mahitaji ya nyumbani, ununuzi wa madawa ya kutibu binadamu, ngamia na wanyma wengine, kuwalipa wachungaji na mengine mengi.

Ngamia hutembea mbali kutafuta malisho na maji kuliko mifugo wengine. Wakiwa malishoni huwa wametawanyika sehemu kubwa na hii huzuia kukanyanga malisho hivyo kuipatia miti na nyasi nafasi ya kunawiri. Tena malisho yaliyo karibu na makazi hupata nafasi ya kustawi. Ngamia wanauwezo wa kustahimili ukosefu wa maji kwa muda mrefu.



## Faida ya ngamia


- Ufugaji wa ngamia ni njia nzuri ya kuwekeza mali na pia ngamia anauwezo wa kustahimili ukame. Bei yake ni nzuri.
- Mapato kutokana na uuzaji wa ngamia hutumika katika miradi kubwa ya familia ambayo haiwezi timizwa na mapato ya mbuzi au kondoo.
- Hutumika pia kwa shughuli za kijamii kama kulipa faini, mahari, sherehe na kadharika.
- Chakula
- Inaaminika maziwa na nyama ya ngamia ni dawa


## Faida ya maziwa ya ngamia dhidi ya maziwa ya mifugo wengine

- Maziwa ya ngamia huchukua muda mrefu kabla hayajaharibika na pia yanaweza kusafirishwa katika mazingira magumu kwa sababu yanastahimili joto jingi.
- Maziwa ya ngamia pia yanaaminika kuwa chakula kinachoponyesha, kwa hivyo ni bidhaa inayopendwa na wengi.
- Maziwa ya ngamia yanaaminika kuwa tiba.


# UZALISHAJI WA NGAMIA


Mfugaji anafaa awe na ngamia mmoja ndume wa umri wa miaka sita hadi kumi na miwili (6-12), na mwingine ambaye hajakomaa atakaye chukua nafasi ya dume huyo atakapozeeka. Dume mmoja anafaa awekwe katika kundi la ngamia kike hamsini. Ndume mmoja ana uwezo wa kuzalisha ngamia kike arobaini hadi sitini wakati kuna malisho ya kutosha.







Unapowachagua dume wa kuzalisha, chagua wanaokua kwa kasi, wenye umbo nzuri la kiume, pia mama yao awe anatoa au aliye na historia ya kutoa maziwa mengi.






Unapowachagua ngamia wa kike, wachague walio na uzoevu wa mazingira, wenye umbo nzuri la kike, (mwili mwembamba na tumbo kubwa, chuchu nne nzuri za maziwa na kiwele kubwa).






Ngamia ndume anapokuwa na joto la kupanda kike, asiruhusiwe kutembea ovyo ovyo kwani anaweza kuumiza  ngamia wa kike au ndama wao.



*Ngamia ndume akiwa tayari kumpanda kike*




*Ngamia ndume akimpanda kike*

Epukana na uzalishaji wa ndume na kike wenye uhusuiano wa karibu wa damu. Ndume aneyetumika kupachika mimba lazima abadilishwe anapofika umri wa miaka kumi na miwili; ambapo mabinti zake wamefikia umri ya kupata mimba.


Usiwatumie ndume ambao wamezeeka katika upachikaji wa mimba kwa sababu huenda mimba hio isifaulu. Ndume chini ya miaka kumi na miwili watumike katika shughuli ya kupachika mimba. Ngamia wa kike anapozeeka, au anapozaa ndama wa sita, anafaa kutolewa katika kundi la ngamia wa maziwa. Ngamia kama huyo hukumbwa na matatizo mengi kama vile: Kuvujika kwa meno, kutoshika mimba kwa haraka na kupungua kwa maziwa.

# NGAMIA ANAPOZAA



Ngamia anapobeba mimba, hakikisha amepata malezi bora na utunzi wa kiwango cha juu. Tenga nyasi au lishe karibu na boma mwezi mmoja kabla ngamia kuzaa. Mchunge ngamia kwa ukaribu ili asije akajifungua akiwa mbali na boma. Ngamia anayetarajia kujifingua asipelekwe kwenye malisho yenye mashimo, mitaro au milima na pia asiwekwe kwenye boma chafu au lenye vumbi.

## Wakati ngamia anapozaa




*Ngamia akizaa*

Ngamia anapozaa, yafaa alale chini kwa boma, pasipo na kelele au usumbufu kwa sababu kelele huchelewesha shughuli ya kujifungua.

Iwapo ngamia anayejifungua atakumbwa na shida ambayo anayemlinda hana ujuzi wa kuitatua, yafaa atafute usaidizi kwa mfugaji mwenye ujuzi au daktari wa mifugo ili kuitatua. Hata hivyo, ni vizuri kujua kuwa mradi ndama yumo tumboni na hajaanza kutoka nje, ndama huyo atakuwa hai kwa muda hata kama mama atakumbwa na shida.


Iwapo kichwa na miguu ya mbele inaonekana, funga Kamba safi katika kila mguu kisha uvute kwa utaratibu. Vile vile, miguu ya nyuma na mkia ikitangulia, funga Kamba kwa kila miguu na uvute polepole. Hakikisha umezingatiwa usafi.



*Ngamia kike akisaidiwa kuzaa*

Ndama huzaliwa akiwa ndani ya kifuko chake cha uzazi. Pasua hicho kifuko pindi tu ndama anapozaliwa iwapo hakitapasuka chenyewe ili ndama aweze kupumua.


Hakikisha kitovu cha ndama kimepakwa kemikali ya iodine. Mweke ndama mbele ya mama mpaka mamake atoe sauti ya kumtambua na kumkubali.



*Ngamia na ndama yake baada ya kuzaa*

Msaidie ndama ili mamake aweze kumwona. Iwapo mama yake atamkataza kunyonya, ambalo ni jambo la kawaida kwa ngamia anayejifungua kwa mara ya kwanza, Muweke umbali wa mama kueza kumwona lakini hamfikii. Pia unaweza kumfunga mama miguu ya nyuma ili kumzuia kumpiga mateke anaponyonya. Hakikisha kondo la nyuma au plasenta imetoka ndani ya tumbo la mama. Kwa kawaida, kondo au plasenta hutoka dakika thelathini baada ya mama kujifungua.
Iwapo plasenta au kondo itakosa kutoka kwa muda, tafuta usaidizi kwa mfugaji mwenye ujuzi au daktari wa mifugo.

# JINSI YA KUTUNZA NDAMA




Ndama anyonye mamake bila kuzuiliwa kwa masaa matatu hadi sita (3-6) ya kwanza baada ya kuzaliwa ilia apate kinga ya mwili, nguvu, protini na vitamini.

Iwapo mamake hatakubali anyonye, basi azuiliwe kisha kiwele na tumbo visuguliwe kwa utaratibu ili kuezesha maziwa kuanza kutoka. Maziwa yakikosekana kabisa, basi ndama apewe maziwa ya ngamia yeyote ambaye amezaa hivi karibuni.


Tibu ugonjwa wa ndama wa kuendasha kwa kumpatia mchanganyiko wa maji, asali/sukari na chumvi ya meza (ya chakula) au utafute usaidizi kutoka kwa daktari wa mifugo aliye karibu. Pia mayai haswa ya kuku anayefugwa karibu na boma ya ngamia yanaweza tumika kama dawa yakipasuliwa. Unapotumia dawa kwa ndama, soma maagizo na uyafuate.

Tenganisha ndama wagonjwa na wenye afya ili kuzuia mambukizi.


## Utunzi wa ndama katika mwaka wa kwanza




Ndama aruhusiwe kufuatana na mama yake popote aendapo kwa kipindi cha miezi mitatu ya kwanza. Wafugaji Hawapaswi kukamua ngamia katika wiki tatu za kwanza.



Kiwango cha maziwa kwa ndama hupunguzwa polepole baada ya mwezi wa tatu ikitarajiwa kuwa ndama ameanza kula nyasi na majani, vilevile afya yake ikizidi kuimarika.







Iwapo mama wa ndama ataaga au ndama akataliwe na mamake, tafuta mama mlezi ambaye atamlea. Ikiwa mama mlezi hapatikani, ndama huyo apewe maziwa ya ngamia mwingine kwa chupa.

Mfugaji azuie ndama kutokana na vimelea kama kupe na wadudu wengine. Anaweza toa kupe akitumia mkono au pia kupaka dawa sehemu zilizoathirika hasa kwa nundu. Tibu jivu mapema kwenye sehemu zilizoathirika kwa kuikata kwa njia inayofaa na pia utumie madawa kama hydrogen peroxide, iodine na aerosol spray ili kuua viini na kuzuia inzi. Hakakisha kupata ushauri wa daktari wa mifugo kuhusu dawa inaysostahili na jinsi ya kuitumia.

## Ndama kuanza kula nyasi na majani peke yake (achishwa)



Ndama azuiliwe kunyonya hatua kwa hatua baada ya kufikisha umri wa kati ya miezi kumi na miwili hadi kumi na minane, kwa kuzingatia kiwango cha mwili, nguvu ya mwili na uwepo wa malisho.




Ndama apewe dawa ya minyoo na pia atibiwe dhidi ya ugonjwa wa malale (trypanosomiasis) kwa dawa inayofaa. Tafadhali pata ushauri wa daktari wako wa mifugo.


Mpe ndama chumvi ya kutosha mara kwa mara. Ongeza kiwango cha maji kwa utaratibu hatua kwa hatua.

Tibu ndama dhidi ya vimelea (parasites) kama vile kupe na sarafu (mange/mites).
Patia ndama chanjo dhidi ya magonjwa kama pepopunda (tetanus) na *clostridia.*
Pata ushauri wa dakatari wa mifugo.

# JINSI YA KUMPATIA NGAMIA LISHE BORA

Mfugaji ampatie ngamia lishe bora kila wakati. Ngamia huchukua muda mrefu akila nyasi na majani. Katika msimu wa mvua, wapelekwe malishoni kwa muda wa masaa nane hadi kumi (8 -10), na wakati wa kiangazi masaa kumi na mawili (12). Lishe bora ni muhimu kwa afya, ukuaji, uzito wa ndama na uzalishaji wa maziwa na nyama.

Ngamia hutawanyika wakiwa malishoni hivyo ni lazima mchungaji awe makini wasipotee au kuliwa na wanyama wa pori. Vile vile mchungaji anafaa ajihadhari na miti au mimea yenye sumu kama vile *capparis tomentosa.* Mimea hii husababisha kifo ngamia wakila.




Ngamia wanapenda sana chumvi na miti yenye chumvi kama vile *indigofera spinosa*. Mahitaji yao ya chumvi ni ya kiwango cha juu kuliko mifugo wengine. Hivyo, mfugaji amupe ngamia wake chumvi mara kwa mara. Mfugaji pia ni bora apeleke ngamia wake mara kwa mara sehemu yenye chumvi asilia. Maji ni muhimu kwa afya ya ngamia, kwa hivyo wapewe maji mara kwa mara. Wakati wa kiangazi ni muhimu wapewe maji baada ya siku tano hadi nane. Muda mrefu zaidi ya siku nane husababisha upungufu wa maji mwilini, maziwa, msongo na kudhoofika kwa mwili. Wakati wa msimu wa mvua ngamia hupata maji kupitia lishe kwa hivyo huchukua muda mrefu kabla ya kunywa maji.

## Utunzaji wa ngamia wenye mimba


Ngamia aliye na mimba apewe majani na nyasi nzuri miezi mitatu ya mwisho kabla hajajifungua. Hilo litafanya ndama aliye tumboni kukua haraka, kuwa na uzito wa juu wakati wa kuzaliwa, na kumpatia mama uwezo wa kutoa maziwa mengi baada ya kuzaa. Ndama anayezaliwa na mama aliyepata lishe bora huwa anakua kwa haraka na huepuka vifo vinavyotokana na uzito wa kiwango cha chini.


Ngamia apate chumvi yenye madini yanayoitajika mwilini kwa kiwango kizuri.

## Utunzi wa ngamia wanaonyonyesha



Ngamia wanaonyonyesha wapate maji yakutosha mara kwa mara na wasikae bila maji kwa muda wa siku sita. Maji ni kigezo muhimu kwa utengenezaji wa maziwa. Ukosefu wa maji husababisha upungufu wa maziwa.






Wapatie ngamia wajawazito na wanaonyonyesha vyakula maalum (vilivyo nunuliwa madukani kama concentrates) haswa wakati wa kiangazi. Wapatie nyasi (hay) au ganda na mbegu za acacia au Mathenge, na pia chumvi yenye madini.

Mara kwa mara, mpime ngamia uzito kwa kutumia kipimo mkanda (tape measure) au kiwango cha uzani (weighing scale). Uzito husaidia kujua kiwango cha dawa cha kumpatia ngamia, wakati wa kumpeleka sokoni au kumchinja na pia unapotaka apachikwe mimba.

Kujua uzito wa ngamia (Kilo) = urefu kutoka bega hadi kwato (SH) x mzunguko wa kifua (TG) x mzunguko wa nundu (AG) x 50.

## Tanbihi

- kipimo ni lazima iwe kwa mita.
- 50 hutumika kwa hiyo fomula kama constant (mara kwa mara).
- Ngamia wapimwe kabla ya kunywa maji.

### Umri wa ngamia

Kujua umri wa ngamia ni jambo la muhimu kwa sababu humwezesha mfugaji kuamua:

- Wakati gani ngamia atapata mimba au atapachikwa mimba.
- Wakati wa kununua au kuuza ngamia.
- Ni ngamia yupi mzuri wa kuuzwa au kuchinjwa.
- Kujua jinsi ngamia anavyonawiri.

Kujua umri wa ngamia kwa kupitia meno ya kato au jembe (incisors) ni muhimu:

- kundi la meno ya kwanza (milk incisors) umri wa miezi miwili (2).
- kundi la meno ya kwanza ya kudumu (permanent incisors) umri miaka 4.5 hadi 5.
- kundi la meno ya kudumu (2rd pair parmanent eruption) miaka 6.
- kundi la meno ya kudumu (3rd pair parmanent eruption) miaka 7 hadi 8.




## Kuweka rekodi na umuhimu wake

Mkulima aweke rekodi ya ngamia wake:

- Rekodi huonyesha kwa jumla picha na historia ya kundi la ngamia.
- Rekodi humsiadia mkulima kufanya uamuzi na mipango muhimu.
- Mkulima atajua wakati wa ngamia kupachikwa mimba, ni ngamia yupi wa kuuzwa, ni wakati gani wa kupeleka ngamia sokoni, ni kiasi kipi cha maziwa ngamia hutoa n.k.
- Rekodi pia humsaidia mkulima kujua kama anapata faida ama hasara katika ufugaji wa ngamia.

# AFYA YA NGAMIA

Ngamia ijapokuwa ni mnyama anayepatikana katika mazingira magumu, anaweza kupatwa na magonjwa kadha wa kadha. Ni muhimu kujua magonjwa tano sugu.



Magonjwa hayo ni:


- Homa ya Bonde La Ufa - Rift valley fever (RVF)
- Ndui ya ngamia-Camel pox
- Ugonjwa wa kuavya mimba ya kuambukiza - Brucellosis
- Kimeta - Anthrax
- Kichaa cha mbwa-Rabies

Mfugaji anashauriwa kuchanja ngamia dhidi ya magonjwa hayo.

Piga marufuku (karantini) kutembea kwa mifugo wakati ugonjwa kama RVF unapotokea.

Ngamia wapewe dawa ya minyoo mara kwa mara.

Mfugaji anashauriwa kuwasiliana na madaktari wa mifugo mara kwa mara pindi tu aonapo dalili yoyote ya ugonjwa. Hii ni muhimu kwa kutambua, kutibu,kuzuia madhara na kuenea kwa magonjwa kwa mifugo wengine.




Ngamia wanapokufa kwa ugonjwa, wazikwe chini ya ardhi au wachomwe haraka iwezekanavyo. Usifunge chuchu za kiwele ili kuzuia ugonjwa wa kititi (mastitis).

## Kutibu vidonda


Vidonda husababishwa na kuumwa, ngozi kukatwa au majeraha ya mwili. Vidonda huwa mbaya zaidi wakati vinapovamiwa na viini kama bakteria.
Mfugaji anafaa aoshe vidonda ili kuondoa uchafu na usaa kabla hajaweka dawa. Vidonda huoshwa kwa kutumia dawa maalum. Pia unaweza kutumia dawa ya kupuliza kwa vidonda ili vipone haraka.

Usifunike au kushona kidonda kichafu ama kilicho na usaa. Kidonda lazima kipone haraka, la sivyo kitaanza kuoza na ngamia atakufa. Vidonda vikioshwa kila siku kwa dawa maalum huwa vinapona haraka, kuliko vidonda vilivyofunikwa na havioshwi. Kudunga sindano pekee haitoshi katika hali ya kutibu vidonda.

Tafadahli pata ushauri wa daktari wako wa mifugo jinsi ya kutibu vidonda katika ngamia wako.

## Kutibu jivu ya ngamia

Sehemu za ngozi zilizofura zitibiwe wakati ngozi ya jivu itakua nyororo (capsules becoming soft). Dakatri wako wa mifugo ataikata sehemu iliyofura kwa njia maalum na kutoa usaha kwa kutumia dawa inayohitajika.  Pia dakatari atakupa mawaidha na kukueleza juu ya dawa nyingine kama vile Kiuavijasumu (antibitoics) inayofaa kutibu kidonda hadi kipone. Shughuli hii ya matibabu itarudiwa kila siku mpaka jivu ipone. Kwa ndama ambao wana shida kama hii katika viungo vyao, daktari wa mifugo atatukueleza dawa inayofaa na muda unaohitajika kwa matibabu hadi kupona.



# JINSI YA KUPATA MAZIWA SAFI YA NGAMIA

Usafi ni jambo la kuzingatiwa ili kupata maziwa safi. Kupata maziwa safi, lazima:

- Ngamia awe safi na mwenye afya
- Mkamuaji awe safi na mwenye afya
- Vyombo vitakavyo tumiwa kwa shughuli ya ukamaji viwe safi
- Mazingira ya kukamlia yawe safi

Kabla ya kuanza kukama ngamia, chukua ndama wake umweke mbele yake. Ngamia akimwona ndama yule, huachilia maziwa. Kama ndama amekufa, tengeneza ama chonga kiyago ama sanamu kisha umfunike na ngozi ya ndama aliyekufa. Ngamia pia anaweza wachilia maziwa akiona mchungaji anayempenda.


Mfugaji akame ngamia mwenye afya na aepukane na ngamia wagonjwa kwa sababu maziwa yao si mazuri kwa matumizi ya binadamu.
Kiwele (udder) na chuchu visiwe na kupe, vidonda au vimefura. Viini (germs) kutoka kwenye vidonda, ama kiwele na chuchu zilizofura uweza kuingia kwenye maziwa na kufanya maziwa hayo kuwa hatari kwa binadamu.

Wachungaji wa ngamia ni lazima waoshe mikono kwa maji na sabuni kabla hawajaanza kukama. Maziwa yaliokamwa bila kuosha mikono, chuchu na kiwele huwa chafu hivyo huharibika haraka na pia yanaweza sababisha magonjwa.

Epukana na maziwa na nyama ya ngamia ambaye anatibiwa mpaka ule muda uliotolewa na daktari uishe, kwa sababu dawa ambazo ngamia hutumia hupatikana kwenye nyama na maziwa kwa muda wa siku kadha na hizi dawa ni sumu kwa binadamu.

Kiuavijasumu (Antibiotics), dawa ya kupe (acaricides), dawa ya minyoo (dewormers) na dawa za malale (trypanocides) zinapotumika kwa nagamia, huathiri maziwa na nyama na kwa hivyo inakuwa sumu kwa binadamu.

## Vyombo vya kukamulia, kuweka na kusafirisha maziwa





Usisafirishe maziwa kwenye mitungi ya plastiki iliyotumika kuweka au kusafirisha vyakula vya binadamu au mafuta ya gari. Mitungi hii mara nyingi huwa na midomo nyembamba, kwa hivyo inakuwa vigumu kuosha vizuri. Ngozi za mitungi kama hizo huwa nyepesi na zina mianya ambayo huficha uchafu. Pia mitungi kuu kuu ya plastiki hutoa kemikali inayoitwa pythalate kwenye maziwa inayosababisha ugonjwa wa saratani na ulemavu wa watoto hasa kwenye viungo vya uzazi.

Maziwa yawekwe na yasafirishwe kwenye ndoo za chuma aina ya alumini (aluminium) zenye vifuniko vizuri. Ndoo za chuma ni nzuri kwa sababu zinaosheka vizuri na pia zinadumu sana hata kama ni bei ghali. Mitungi ya plastiki ndio chanzo cha maziwa kuharibika na kumwagika yanaposafirishwa. Mitungi hii hudumu kwa muda mfupi sana.

Funga (wrap) ndoo ya maziwa kwa kitambaa chenye unyevunyevu ili maziwa yapate baridi. Ni vizuri uweke ndoo zenye maziwa kwenye kivuli au ndani ya jokofu (fridge) kabla ya kuyasafirisha mwendo mrefu. Maziwa baridi hukaa muda mrefu kabla ya kuharibika.



Kuna baadhi ya vyombo vya kitamaduni vya kubebea maziwa kama vile vya kisomali (Somali haan) vikikaushwa na moto vizuri, basi hukubalika kuweka na kusafirisha maziwa. Vina sifa nzuri Sana ya kufanya maziwa kuchacha. Kuna baadhi ya miti ambayo hutumika kukausha vyombo vya kitamaduni za kubebea maziwa. miti hii ni kama;- olea Africana, Balanites aeqyptica, Diplorhynchus condylaccaepon, Combretum ssp.
Usichanganye maziwa yaliokamwa mapema na yale yaliokamwa sasa. Maziwa ambayo yamekaa Sana yanaweza haribu maziwa mazuri.

## Jinsi ya kutunza maziwa.


- Ngamia wanaokamwa wawe safi na wenye afya.
- Ngamia wenye afya nzuri kwanza wakamwe wakifuatwa na ngamia wasio na afya nzuri.
- Tumia mikebe midogo safi iliyooshwa kwa maji moto au kemikali zinazofaa wakati wa kukama.
- Wanaowakama ngamia lazima wawe ni watu wenye afya, nguo safi na kila wakati wazingatie usafi wa hali ya juu.
- Funika maziwa baada ya kukama ili kuzuia kuchafuka.
- Ndoo za kusafirisha maziwa lazima ziwe safi kila siku kabla na baada ya kusafirisha.

## Kuosha na kuua vijidudu (germs) kwenye vyombo vya kukama

- Vyombo vyote kama vile, mikebe, ndoo na chupa zioshwe vizuri kwa maji moto,sabuni na kemikali spesheli.

## Utaratibu wa kuosha





- Nawa mikono kwa sabuni na maji mengi kisha uikamue.
- Tumia makonge au kitaambaa pamoja na sabuni ya kuosha vyombo.
- Tumia maji mengi kuosha vyombo kisha kukamua vizuri.
- Tia vyombo kwenye maji yanayochemka kuua viini (germs).
- Baadaye anika vyombo nje,shehemu ya njuu ikiangalia chini, pahali wazi ,kwenye jua, juu ya meza au kitu kilichotengenezwa cha kuanikia vyombo safi .
- Ifadhi vyombo hivi mahali safi.

## Changamoto katika ufugaji wa ngamia

- Magonjwa ya ngamia kama vile malale (trypanosomiasis), *heamorrhagic septicaemia*, rye neck, camel sudden death nk.
- Uvamizi wa kupe(vimelea) na wadudu wengine.
- Vifo vya ndama kutokana na magonjwa kama vile kuhara na pia ukosefu wa maziwa ya kutosha.
- Uaviaji wa mimba na ndama kuzaliwa kabla wakati unaofaa.
- Kushambuliwa na wanyama wa pori.
- Wizi wa mifugo au ngamia kupotea
- Kutoweza kushika mimba au kukaa muda mrefu bila kushika mimba.
- Wachungaji wasumbufu au au uhaba wa wachungaji hodari/wazuri
- Miti yenye sumu malishoni kama vile capparis tomentosa(laturdei kwa kisamburu)
- Uhaba wa maafisa wa nyanjani
- Ukame wa mara kwa mara

# MAREJELEO:

George Karuoya Gitau, Peter Kimeli, Davis Ikiror, Willy Mwangi, Douglas Machuchu, Moses Irungu Gakuru, and Genevieve Owuor (2022): Factors associated with total coliform and total viable bacterial count in camel milk from Isiolo County, Kenya
Veterinary World, 15(8): 1954-1960

Vétérinaires Sans Frontières Suisse (2014): Guidelines for the Training of Veterinary Professionals on Camel Health and Diseases ISBN 9966-956-85-9

Kenya Camel Association (2012): Camel Manual for Service Providers (Revised Edition 2012): Compiled and edited by Ngeiywa K. Juma, Nyanja C.J., Toroitich Charles Kisa, Khalif A. Abey, Wamwere-Njoroge, Guliye A.Yakub. ISBN 9966-05-284-4

H. J. Schwartz, Maurizio Dioli (Editors:) (1992): The One-Humped Camel in Eastern Africa. A pictorial guide to diseases, health care and management. Publisher: Verlag Joseph Margraf ISBN: 3-8236-1218-2

Peter Obimbo Lamuka, Francis M. Njeruh, George C. Gitao and Khalif A.Abey (2017): Camel health management and pastoralists' knowledge and information on zoonoses and food safety risks in Isiolo County, Kenya. Pastoralism volume 7, Article number: 20 (2017)

ISBN 978-9914-49-227-9

9 789914 492279